**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
**DODOMA.**

**14 Mei, 2024**

## YALIYOMO

**ORODHA YA VIELELEZO** .......... **ii**
**SEHEMU YA KWANZA** .......... **1**
**1.0 UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Maelezo ya Jumla .......... 1
1.2 Msingi wa Uchambuzi na Uwasilishaji wa Taarifa Hii .......... 2
1.3 Mawanda ya Uchambuzi na Taarifa .......... 3
**SEHEMU YA PILI** .......... **5**
**2.0 MAELEZO KAMILI KUHUSU UCHAMBUZI NA TATHMINI** .......... **5**
2.1 Ufafanuzi wa Jumla .......... 5
2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 .......... 5
2.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida .......... 14
2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati .......... 16
2.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 .......... 17
**SEHEMU YA TATU** .......... **24**
**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** .......... **24**
3.1 Ufafanuzi wa Jumla .......... 24
3.2 Maoni na Ushauri wa Jumla .......... 24
3.3 Maoni na Ushauri Maalum Kisekta .......... 26
3.4 Sekta ya Mifugo .......... 26
**4.0 HITIMISHO** .......... **31**
3.5 Shukrani .......... 32

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024 ..........................6
Kielelezo Na. 2: Mwenendo na mtririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2023/2024......8
Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2024 ......................15

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Msingi wa Uchambuzi, Muundo wa taarifa na njia zilizotumika kutekeleza jukumu la kushughulikia bajeti hii;

(ii) Sehemu ya Pili inatoa maelezo kamili kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri kutokana na uchambuzi na kuhitimisha maudhui ya Taarifa hii.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi na Uwasilishaji wa Taarifa Hii

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(1)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yaliyoitaka Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, yaliitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024 ili kulinganisha na Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Kamati za Kisekta kuchambua Taarifa za Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, shughuli ya Bunge kujadili hoja hii leo imestahili kutanguliwa na uchambuzi kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 184 (5) ya Kanuni za Bunge, Waziri Mtoa Hoja na Kamati hii tulitakiwa kuweka mezani nakala ya Taarifa zinazohusika kabla ya kuanza mjadala. Nafurahi kwamba, mapema asubuhi, nakala ya Taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Aidha, Kanuni ya 184 (6) ya Kanuni za Bunge imetaka maoni ya Kamati yatolewe Bungeni baada ya Waziri anayehusika kuwasilisha hotuba yake. Ninashukuru kwamba, kwa sasa, tumepewa nafasi ya kuiwasilisha Taarifa hii ili iweze kuzingatiwa na Bunge wakati wa kujadili hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi na Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaoripotiwa katika Taarifa hii unagusa utekelezaji wa bajeti katika Mafungu mawili; **Fungu 99** Sekta ya Mifugo na **Fungu 64** Sekta ya Uvuvi kwa mwaka 2023/2024. Aidha, kwa upande wa Makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025 uchambuzi umefanyika kwa **Fungu 99** - Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Hali hiyo imezingatia uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Makadirio ya Sekta ya Mifugo na

Sekta ya Uvuvi chini ya **Fungu moja 99** – Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla wake, uchambuzi huu umegusa mambo makuu yafuatayo:-

(i) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
(ii) Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;
(iii) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;
(iv) Tathmini ya Ukusanyaji wa maduhuli; na
(v) Upatikanaji wa fedha kutoka hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) iliyotaka matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti yatumike kufanya ulinganisho na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo uliiwezesha Kamati kupata mambo ya kuzingatia kuhusu hoja inayojadiliwa leo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO KAMILI KUHUSU UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 21 Machi, 2024 Kamati ilikutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika maelezo hayo Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa majukumu, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

#### 2.2.1 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, **Sekta ya Mifugo** - Fungu 99 ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 42,105,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 17,330,279,726** sawa na

**asilimia 41.16** ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi Fungu 64 lengo lilikuwa ni kukusanya jumla ya **Shilingi 41,000,000,000** kutoka vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa katika Taarifa. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 17,897,169,912.78** ambayo ni sawa na **asilimia 43.7** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua maduhuli hayo kwa kila fungu ili kujiridhisha na juhudi za ukusanyaji wa maduhuli. Matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika **Kielelezo Na. 1**.

**Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024**

| Fungu | Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024 | Makusanyo ya Maduhuli hadi Kufikia Februari, 2024 | Asilimia ya Makusanyo |
|---|---:|---:|---:|
| **Fungu 99** – Sekta ya Mifugo | **42,105,000,000** | **17,330,279,726.00** | 41.16 |
| **Fungu 64**- Sekta ya Uvuvi | 41,000,000,000 | 17,897,169,912.78 | 43.7 |
| **JUMLA KUU** | **83,105,000,000** | **35,227,449,639** | **42.4** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 99 na Fungu 64*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Jumla ya makusanyo ya maduhuli hadi kufikia Februari, 2024 yamefikia **asilimia 42.4** ya lengo;

(ii) Sekta ya Mifugo iliyokadiriwa kuchangia **asilimia 51** ya makusanyo ya Wizara imechangia **asilimia 49**; na

(iii) Sekta ya Uvuvi iliyokuwa imekadiriwa kuchangia **asilimia 49** ya makusanyo imechangia **asilimia 51**;

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya ukusanyaji wa maduhuli inaonesha kuwa ni vigumu kwa Wizara kufikia lengo lililowekwa la ukusanyaji wa maduhuli. Aidha, pamoja na ukusanyaji usio na mwelekeo wa kufikia lengo, Sekta ya Uvuvi imejitahidi ikilinganishwa na Sekta ya Mifugo.

### 2.2.2 Mwenendo na Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa kiasi cha **Shilingi 194,335,967,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Shilingi 165,274,198,000.00**; na Fedha za Nje ni **Shilingi 29,061,769,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024, Wizara ilipokea **asilimia 41.56** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hiyo inaonesha kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho ulikuwa nyuma kwa **asilimia 58.4. (Kielelezo Na. 2).**

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo na mtririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2023/2024**

| MTIRIRIKO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO HADI FEBRUARI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **MIRADI** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2023/2024** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2024** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| Fedha za Ndani | **165,274,198,000.00** | | |
| Fedha za Nje | **29,061,769,000.00** | **80,820,027,430.46** | **41.56** |
| **Jumla** | **194,335,967,000.00** | | |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, ni wazi kuwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na Serikali kupitia Wizara hii haiwezi kufikiwa. Hali hii sio nzuri na inaweza kusababisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi kushindwa kuchangia vyema katika pato la Taifa, kukuza ajira na kupunguza umasikini miongoni wa Watanzania waliojiajiri kupitia Sekta hizi.

### 2.2.3 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu (3) ya Tanga, Dar es Salaam na Pwani na kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Miradi hiyo ni: -

(i) Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo katika mpaka wa Horohoro, Tanga (Mradi Na. 4486);

(ii) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi Tanzania -(TAFICO); na

(iii) Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo lililopo Vikuge, Kibaha Mkoa wa Pwani.

### 2.2.4 Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo, Horohoro, Tanga (Mradi Na. 4486)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo, Horohoro, Tanga una thamani ya **Shilingi 563,079,225.12**. Mradi unalenga kudhibiti utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani kupitia Mpaka wa Horohoro pamoja na kuimarisha biashara ya mifugo nchini. Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mnada huo umeanza kutumika kuanzia mwezi Septemba, 2023, ambapo hadi sasa umechangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha **Shilingi 9,428,650**. Aidha, idadi ya mifugo iliyouzwa katika mnada huo ni **809** ikijumuisha ngómbe **359**, mbuzi na kondoo **450**. Vile vile mifugo **278** imesafirishwa kwenda nje ya nchi ikiwemo ngómbe **134** na mbuzi **144**.

### 2.2.5 Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya TAFICO Makao Makuu ulihusisha ununuzi wa mtambo wa barafu, ujenzi wa kibanda na ununuzi wa kengevuke. **Shilingi 1,000,000,000.00** zimeidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, hadi sasa mradi umetekelezwa kwa **asilimia 49.** Mradi huu unalenga kuongeza ajira na mapato ya fedha za ndani na za kigeni yatakayowezesha kukuza pato la Taifa. Pamoja na hayo, TAFICO inatarajiwa kuongeza uhamasishaji wa Sekta Binafsi ili kuwekeza zaidi katika uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji, uchakataji pamoja na mauzo ya mazao ya uvuvi hapa nchini kwa kutumia mbinu na teknolojia za kisasa.

**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji huu ni muhimu kwa kuwa utaiwezesha nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Miliki (*Exclusive Economic Zone-EEZ*) na Bahari Kuu. Kwa sasa uvuvi kutoka eneo letu la EEZ unafanywa na meli za kigeni.

### 2.2.6 Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo - Vikuge Mkoani Pwani

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mradi huu unalenga kuimarisha uzalishaji wa mbegu na malisho kwa lengo la

kuongeza upatikanaji wa mbegu na malisho kwa wafugaji.

**Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelezwa hadi sasa katika Mradi huu ni pamoja na kusafisha pori lenye ukubwa wa **hekta 175** kwa thamani ya **Shilingi 160,539,000.** Jumla ya **hekta 100** kati ya **175** zilisafishwa na kufikia **asilimia 65** ambapo Hati Na. 1 yenye thamani ya **Shilingi 84,063,200** iliwasilishwa Wizarani kwa ajili ya malipo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuzalisha mbegu na malisho (*hay and silage*) ili kuongeza upatikanaji wa malisho, kutoa elimu na kuwajengea uwezo wafugaji kuhusu namna bora ya kuzalisha na kuhifadhi. Aidha, mbegu na malisho yatakayozalishwa yatauzwa kwa wafugaji na wazalishaji binafsi ili kuuwezesha Mradi kujiendesha na kuufanya uwe endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo yameonesha mambo yafuatayo:-

**(a) Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo - Horohoro, Tanga (Mradi Na. 4486);**

(i) Kumekuwa na utoroshwaji wa mifugo kwa kupitia njia za panya kwenda nchi Jirani ya Kenya. Aidha, bado idadi ya mifugo inayouzwa katika Mnada wa Horohoro ni ndogo, jambo linalopunguza mapato ya Serikali;

(ii) Ushuru wa mifugo kwenye Mnada wa Horohoro ni mkubwa ambapo ng'ombe mmoja anatozwa **Shilingi 30,000,** hali inayochochea utoroshwaji wa mifugo kupitia njia za panya;

(iii) Pamoja na Halmashauri ya Mkinga na Serikali ya Kijiji kutoa eneo la kujenga mnada bado hawanufaiki na mapato yanayotokana na mnada huo. Hali hii inatokana na utaratibu wa Serikali kuu kuchukua mapato yote yanayotokana na mnada;

(iv) Kukosekana kwa ulinzi katika eneo la mnada kunahatarisha usalama wa watu, mifugo na majengo wakati na baada ya shughuli za uuzaji wa mifugo;

(v) Kukosekana kwa majengo ya ofisi, Kituo cha Polisi na miundombinu ya maji katika eneo la mnada, kunahatarisha usalama na afya za watumiaji wa mnada huo; na

(vi) Pamoja na eneo la mnada kuwa kubwa, hakuna mpango wowote wa kuwa na malisho ya mifugo wakati wafugaji wakiwa wanasubiri kuuza mifugo yao.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto hizo ni dhahiri kuwa lengo la Mradi kuimarisha biashara ya Mifugo na kuongeza mapato haliwezi kufikiwa. Kamati ina maoni kwamba, changamoto hizo zinapaswa kutatuliwa.

**(b) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi - TAFICO**

(i) Baadhi ya majengo ya TAFICO yaliyo pembezoni mwa Bahari yako hatarini kuanguka kutokana na maji kula kingo za ardhi;

(ii) TAFICO kukabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo na upungufu wa zana za kutosha kama vile meli za uvuvi; na

(iii) Mtiririko usioridhisha wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hali hiyo inasababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ni vigumu kwa Taasisi hiyo kufikia dira yake ya kuwa Kituo Bora cha Utafiti na Ushauri Elekezi katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika. Aidha, TAFICO haitoweza kuendeleza uvuvi wa kibiashara na Sekta ya Uvuvi nchini kama ilivyokusudiwa.

**(c) Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo - Vikuge Mkoani Pwani**

(i) Ukosefu wa miundombinu ya kukaushia na kuhifadhia mbegu za malisho, hali inayosababisha upotevu wa malisho na mbegu kuharibika;

(ii) Ukosefu wa miundombinu ya kuhifadhia malisho baada ya kuvunwa na kabla ya kuuzwa kwa

wanunuzi, hali inayochangia hasara kutokana na malisho kuharibika;

(iii) Ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji, hali inayosababisha shamba kupunguza uzalishaji hasa kipindi cha kiangazi; na

(iv) Uchakavu wa mitambo/vifaa ikiwemo trekta, mashine za kukata majani (*mower*), *bailer, hay rake,* hali inayoathiri ufanisi na tija katika shamba hilo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo, tija ya mradi na manufaa kwa wafugaji hayawezi kupatikana inavyostahili. Kamati ina maoni kuwa, ipo haja ya kuongeza usimamizi wa Mradi huu kwa lengo la kusaidia manufaa makubwa kwa wafugaji. Aidha, Serikali itapaswa kutoa fedha za utekelezaji wa Mradi huu ili kuendelea kupata tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuendelea kuwafikishia wananchi miradi mbalimbali ambayo ina lengo la kutatua changamoto zinazowakabili hasa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

### 2.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Sekta za Mifugo **(Fungu 99)** na Uvuvi **(Fungu 64)** zilitengewa jumla ya **Shilingi 292,520,933,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida

na kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye **Kielelezo Na. 3**.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2024**

| UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU (99&64) HADI FEBRUARI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2023/2024** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2024** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| Mishahara | 39,308,758,000.00 | 20,800,000,000.00 | 52.91 |
| (OC) | 58,876,208,000.00 | 17,050,000,000.00 | 28.86 |
| **Jumla** | **98,184,966,000.00** | **37,850,000,000.00** | **38.55** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Sekta ya Mifugo - Fungu 99 na Sekta ya Uvuvi - Fungu 64***

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilipokea **asilimia 38.55** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Matumizi ya Kawaida;

(ii) Pamoja na kuwa Sekta ya Uvuvi ilikadiriwa asilimia 49 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara, lakini Sekta hiyo ilipokea asilimia 30 ya fedha zilizopokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida; na

(iii) Sekta ya Mifugo iliyokadiriwa kupata fedha za matumizi ya kawaida, imepata **asilimia 69** ya fedha kidogo za Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha, Sekta zote mbili yaani Sekta ya Uvuvi na Sekta ya Mifugo hazitarajiwi kukamilisha majukumu yake yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Pamoja na kuwa mwenendo wa jumla unaonesha hali ngumu ya upatikanaji wa fedha, Sekta ya Uvuvi imekabiliwa na hali ngumu zaidi ikilinganishwa na Sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo inahatarisha mchango wa Sekta hizo katika Uchumi wa Taifa. Aidha, hali hiyo inaathiri ustawi wa watu ambao shughuli zao kuu za uchumi zimeegemea katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kamati ina maoni kuwa upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki kwa ajili ya Sekta hizo zinapatikana kabla ya tarehe 1 Julai, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Mifugo na Uvuvi ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

### 2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali

imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu uendeshaji wa Vituo vya BBT na ufugaji bora wa kisasa. Taarifa za Wizara zilionesha kuwa Vituo vya BBT vimeanzishwa na Vijana waliopo katika Vituo hivyo wanafundishwa mbinu za ufugaji bora ili kuzalisha mifugo inayokidhi mahitaji ya soko la ndani na la nje.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri, yapo maeneo mengine ya ushauri wa Kamati hayajafanyiwa kazi inavyostahili. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa Serikali ianzishe Mamlaka mpya ya Usimamizi wa Miradi ya Wizara hii lakini taarifa ya Wizara inaonesha kwamba, hatua iliyofikiwa ni maandalizi ya andiko la kuanzisha Chombo Maalum.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na hatua hiyo kwa kuwa ilitimia miezi isiyopungua nane tangu ushauri kutolewa na Wizara kuendelea kuwa kwenye andiko. Athari yake ni kusababisha fedha za Serikali kupotea, miradi kutokuwa na tija na wananchi kutonufaika na miradi hiyo kama ilivyokusudiwa.

## 2.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi - **Fungu 99** imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako

Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 kama ifuatavyo: -

### 2.5.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa Makadilio ya Maduhuli yaliyopangwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi - **Fungu 99.** Ili kujenga msingi wa maoni na ushauri kuhusu Maduhuli, Kamati ilichambua maduhuli hayo kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara hii yamepungua kwa **asilimia 14.56** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024;

(ii) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024, lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 halina uwezekano wa kutimizwa. Sababu za mtazamo huo hadi kufikia kipindi cha takribani **asilimia 66** ya muda wa utekelezaji, lengo lilifikiwa kwa **asilimia 42.4** tu. Kasi hiyo ya ukusanyaji ilikuwa nyuma ya lengo kwa **asilimia 24** lakini punguzo la lengo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 halifiki **asilimia 24**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kawaida makadirio ya jumla ya bajeti ya nchi, huzingatia makadirio ya makusanyo kwa Sekta moja moja. Uwekaji wa lengo la makusanyo usiozingatia uhalisia unaweza kuathiri uhalisia wa bajeti ya matumizi. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa, ni vizuri kila Sekta inapokadiria ukusanyaji wa maduhuli izingatie uhalisia.

### 2.5.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha majukumu ya Wizara, makadirio ya Bajeti kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni jambo muhimu. Kutokana na hivyo, Kamati ilichambua makadirio ya Matumizi ya **Fungu 99** – Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio yamepungua kwa **asilimia 2** ukilinganisha na mwaka unaoisha;
(ii) Kutokana na uzoefu wa upatikanaji wa fedha wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaokwisha, kiasi cha fedha kinachokadiriwa kwa matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 kinaweza kisipatikane kama inavyoombwa; na
(iii) Makadirio ya matumizi kwa Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi yamejumuishwa katika Fungu moja – **Fungu 99** - Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Uzoefu huu ni tofauti kabisa na mwaka wa fedha 2023/2024

ambapo kila Sekta ilikuwa na Fungu linalojitegemea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kubaini kuwa bajeti ya Wizara hii ilipaswa kuendelea kuongezwa. Sababu yake ni kuwa, Ilani ilitambua umuhimu wa kuongeza tija katika ufugaji na uvuvi kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha tofauti na matarajio hayo ya Ilani. Ni maoni ya Kamati kwamba, Sekta ya Uvuvi na Mifugo zinapaswa kupewa kipaumbele.

### 2.5.3 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, uendelezaji wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kiasi kikubwa unategemea bajeti inayopangwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo chini ya sekta hizo. Kwa madhumuni ya kupata mwelekeo katika Sekta hizo, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa **asilimia 79** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024;

(ii) Utegemezi wa vyanzo vya nje kwa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umeongezeka kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na mwaka wa fedha

2023/2024. Katika mwaka wa fedha unaoisha **asilimia 15** ya bajeti ya maendeleo ilikuwa ni fedha za nje lakini kwa mwaka 2024/2025 **asilimia 32** ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje.

(iii) Pamoja na kuwa uhakika wa upatikanaji wa fedha za nje kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulithibitika kuwa mdogo, ongezeko la uwiano wa fedha za nje haliendani na uhalisia uliojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha wa 2023/2024. Kwa mfano, Sekta ya Mifugo ilipokea **asilimia 0.7** ya makadirio ya fedha za nje; na

(iv) Uzoefu wa jumla wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kuwa, katika kipindi cha utekelezaji cha **asilimia 66,** Wizara ilipata fedha za maendeleo kwa kiasi cha **asilimia 41** ya makadirio. Kwa hali hiyo, uzoefu umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha umekuwa mgumu kwa **asilimia 25**. Hali hiyo inathibitisha kuwa ongezeko la bajeti kwa **asilimia 79** linaweza lisiwe na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yana sura ya kuongeza ufanisi katika Sekta hizo. Hata hivyo, iwapo changamoto za upatikanaji wa fedha zilizojitokeza katika mwaka wa fedha ulioisha hazitapatiwa ufumbuzi, makadirio haya yanaweza yasiwe na maana. Kamati ina maoni kuwa, upo

umuhimu wa Serikali kuongeza mkazo katika upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo chini ya Sekta hizi.

### 2.5.4 Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** ili kubaini matokeo ya bajeti inayojadiliwa Fungu 99, Kamati ilifanya mapitio ya maeneo ya vipaumbele katika bajeti ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na mapitio hayo Kamati ilibaini kuwa:-

(i) Maeneo yote ya vipaumbele yaliyobainishwa na Wizara yanaendana na mwelekeo wa nchi na mahitaji ya jamii;

(ii) Iwapo vipaumbele hivyo vitazingatiwa ipasavyo, Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi zitaongeza mchango katika Uchumi wa Taifa, maendeleo ya nchi na ustawi wa watu nchini; na

(iii) Iwapo upatikanaji wa fedha zitakazoidhinishwa kutokana na makadirio hayo utakuwa wa kusuasua, vipaumbele hivyo vitabaki na mwonekano unaovutia lakini usiokuwa na tija.

**Mheshimiwa Spika**, kwa vipaumbele hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inastahili pongezi kwa nia yake ya kuboresha Sekta hiyo. Aidha, Serikali kwa ujumla wake inahitaji kuzingatia umuhimu wa vipaumbele hivyo ili kuboresha zaidi Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwa lengo la kupata mchango mkubwa katika Uchumi wa nchi. Kwa

mtazamo huo, ipo haja ya kusisitiza zaidi upatikanaji wa fedha zinazoombwa wakati wa utekelezaji, mbali na hivyo, mchango wa Sekta hizo utakuwa mashakani.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kuliwezesha Bunge kujadili Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa namna yenye manufaa kwa Taifa. Ili kufanikisha lengo hilo, Kamati imezingatia matokeo ya uchambuzi na tathmini na kutoa maoni na ushauri kwa namna mbili; ya kwanza ni maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali na ya pili ni maoni na ushauri kwa kila Sekta.

### 3.2 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, maoni na ushauri katika sehemu hii, unatokana na kuzingatia vipaumbele vilivyobainishwa na Wizara kwa kulinganisha na hali halisi ya Sekta. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kama ifuatavyo:-

(a) Wingi wa Tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi unakwamisha maendeleo ya Sekta hizo nchini na kusababisha maisha ya wafugaji na wavuvi kuendelea kuwa duni. Ili kutatua changamoto hiyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kupunguza tozo ambazo ni kero na vikwazo kwa maendeleo ya Sekta hizo na kusababisha umasikini kwa wafugaji na wavuvi;

(b) Mtiririko usioridhisha wa fedha kutoka hazina, hususan fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo umekwamisha

utekelezaji wa miradi hiyo ukiwemo mradi wa BBT (Mifugo na Uvuvi). Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe kwamba Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii zinapatikana kwa wakati;

(c) Utaratibu wa kuanzisha miradi mingi kwa pamoja na kushindwa kuikamilisha, na usimamizi hafifu wa utekelezaji unachangia matokeo yasiyoridhisha ya miradi kaitka Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Ili kukabiliana na changamoto hii Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

   (i) Serikali iweke na kuzingatia vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ili ikamilike kwa wakati na kuepuka ongezeko la gharama za miradi;

   (ii) Iandaliwe mikakati ya kusimamia miradi kikamilifu ili tija iliyokusudiwa ipatikane;

(d) Kukosekana kwa Mamlaka za Usimamizi wa Utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni jambo linalochangia kuzorota kwa Sekta hizo. Aidha, hali hiyo inapunguza mchango wa Sekta za uvuvi na mifugo katika Pato la Taifa, ustawi wa watu na maendeleo kwa ujumla. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ikamilishe mchakato

wa kuanzisha Mamlaka Mpya za Sekta za Mifugo na Uvuvi.

### 3.3 Maoni na Ushauri Maalum Kisekta

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutimiza jukumu lake la kuishauri Serikali, Kamati imezingatia tathmini ya jumla ya kila Sekta chini ya Wizara hii na kuilinganisha na hali halisi. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo yanaisukuma Kamati kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

### 3.4 Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Spika**, Katika Sekta ya Mifugo Kamati ina maoni na ushauri kama iufuatavyo:-

(a) Utoroshwaji wa Mifugo kwa njia za panya ni jambo lisilofaa kwa uchumi wa nchi. Hali hiyo inaikosesha Serikali mapato, na kuvuruga takwimu muhimu kwa ajili ya mipango ya nchi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Kamati inashauri kwamba:-

(i) Minada ya mifugo ijengwe katika maeneo ya mipakani na iwekewe ulinzi ili kudhibiti utoroshwaji wa mifugo kwenda nje ya nchi;

(ii) Ushuru unaotozwa katika minada ya mifugo ufanyiwe mapitio kwa lengo la kubaini kiwango cha ushuru kinachoweza kuwavutia wafugaji kuuza mifugo yao kwenye minada hiyo;

(iii) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe kwamba Halmashauri

nchini zinaweka mikakati ya kulinda maeneo yote ya Mipaka ili kuzuia utoroshwaji wa mifugo. Aidha, Halmashauri za Wilaya na Vijiji zinufaike na mapato yatokanayo na minada iliyopo kwenye maeneo yao.

(iv) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, isukume mazungumzo miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kukubaliana namna bora ya kutumia minada ya mifugo ya mipakani.

(b) Uhaba wa malisho hasa kipindi cha ukame unaathiri mifugo na kusababisha Wafugaji walazimike kutafuta malisho kwa kuhamahama. Hali hii inachangia kupoteza ubora wa mifugo, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na uharibifu wa mazingira. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kwamba:-

(i) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya uanzishwaji wa maeneo ya mashamba ya malisho na mbegu za malisho;

(ii) Miundombinu ya mashamba ya mbegu na malisho iboreshwe ili kuongeza tija katika uzalishaji. Aidha, barabara zinazofika kwenye mashamba ya mbegu na malisho ziboreshwe ili ziweze kupitika wakati wote;

(iii) Serikali itengeneze miundombinu ya kukaushia malisho katika mashamba ili kudhibiti upotevu.

Sambamba na hilo, maghala ya kuhifadhia malisho baada ya kuvunwa yajengwe na kuendelezwa; na

(iv) Serikali ijenge miundombinu ya umwagiliaji, ili kuhamasisha na kuongeza uzalishaji wa malisho hasa kipindi cha kiangazi;

(c) Kutofanyika kwa utambuzi wa mifugo, kunasababisha dosari katika udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, uimarishaji wa usalama wa chakula, dosari za udhibiti wa biashara ya mifugo na mazao yake na udhibiti duni wa wizi wa mifugo. Ili kutatua tatizo hilo, Kamati inashauri kwamba Serikali ifanye utambuzi (sensa) ili kujua takwimu sahihi za aina, idadi, mtawanyiko wake na taarifa nyingine muhimu zinazohusu mifugo nchini. Aidha, Serikali ihakikishe inasimamia utoaji wa Chanjo ya mifugo nchi nzima.

### 3.4.1 Sekta ya Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Uvuvi Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Uhaba wa Samaki katika Bahari, Maziwa, Mabwawa na mito unasababishwa kwa kiasi kikubwa na Uvuvi Haramu ambao unaathiri mazalia na biashara ya Samaki nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kuwa, Serikali iwahamasishe wadau na Sekta binafsi kushiriki katika udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya samaki;

(b) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (*Post - harvest losses*), unaokadiriwa kufikia asilimia 30 hadi 40 hususan katika maeneo ya vijijini. Upotevu huu umesababisha Sekta hii kutochangia ipasavyo katika Pato la Taifa tofauti na ukubwa wake. Kamati inashauri kuwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itoe elimu ya namna ya kuhifadhi mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa. Aidha, Wizara ijenge miundombinu ya kuhifadhia samaki kama vile vituo vya kuzalisha barafu katika maeneo ya uvuvi.

(c) Sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu yanapotea kutokana na ukosefu wa nyenzo za uvuvi katika eneo hilo. Aidha, njia ya kukabiliana na ukosefu wa nyenzo kwa kutoa leseni kwa meli za kigeni inaongeza upotevu wa mapato. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kununua meli nne za uvuvi ili zisaidie kufanya uvuvi kwenye eneo la bahari kuu na kuongeza mapato ya nchi;

(ii) Serikali iendelee kuimarisha doria za mara kwa mara kwenye eneo la Uvuvi la Bahari Kuu ili kudhibiti uvuvi haramu;

(iii) Serikali ishirikishe Sekta Binafsi na kuiwekea mazingira rafiki kwa ajili ya ujenzi wa viwanda

vya uchakataji na usindikaji wa mazao ya uvuvi ili kukuza mchango wa Sekta katika Pato la Taifa;

(iv) Serikali iongeze bajeti ya TAFICO na kuliwezesha kupata watumishi wa kutosha ili Shirika hilo liweze kutekeleza majukumu yake inavyostahili; na

(v) Uhaba wa vifaranga vya Samaki na chakula bora cha samaki nchini unarudisha nyuma juhudi za Serikali kuhamasisha wananchi kujikita katika ufugaji wa Samaki. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ishirikishe Sekta Binafsi katika uzalishaji wa chakula na vifaranga vya samaki kwa gharama nafuu ili kusaidia kuhamasisha wananchi hasa vijana kujikita katika ufugaji wa samaki wa vizimba, kupunguza tatizo la ajira na kuongeza pato la Taifa.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, Sekta za Mifugo na Uvuvi ni za uzalishaji ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa Sekta ya Viwanda. Aidha, Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Ibara ya 9(C), ukurasa wa 7, Serikali iliahidi Kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika Ibara ya 43 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ukurasa wa 54, Serikali imeahidi kuimarisha Sekta ya Uvuvi kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili iweze kuhimili ushindani na kuifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuachana na uagizaji kutoka nje pamoja na kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025) na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mifugo inachangia **asilimia 7** ya Pato la Taifa. Pato hilo linatokana na uzalishaji wa nyama ya ng`ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, Sekta ya Uvuvi inachangia takribani **asilimia 1.8** ya pato la Taifa. Zaidi ya Watanzania **milioni 4.5** wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali zikiwemo kuunda na kutengeneza

boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na Baba na Mama lishe. Aidha, Sekta ya Uvuvi huchangia **asilimia 30** ya protini inayotokana na mazao ya wanyama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, endapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi itapewa fedha ya kutosha kwa ajili ya kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii ina uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa, hali itakayopelekea Wafugaji kunufaika na mifugo yao.

### 3.5 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao, natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda, naomba yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Deodatus Mwanyika, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Mzuzuri, Mb, - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb

5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb
6. Mhe. Dkt. Christine Ishengoma, Mb
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb
10. Mhe. Dkt. Medard Kalemani, Mb
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
19. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
20. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
21. Mhe. Toufiq Salim Turky, Mb
22. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb
23. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
24. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb


**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mhe. Abdallah Ulega (Mb) na Naibu Waziri - Mheshimiwa Alexander Mnyeti (Mb), kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo yake wakiongozwa na Katibu Mkuu - Prof. Riziki Shemdoe, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Mhe. Deodatus Phillip Mwanyika
**MWENYEKITI**
KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA,
BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO

14 MEI, 2024